

Washiriki wakuu wa IntHEC



Liverpool School of Tropical
Medicine LSTM, UK
Consortium Coordinator



Wizara ya Elimu na Ufundi,
(MoEVT), Tanzania



Université Catholique de
Louvain UCL, Belgium



Laboratoire d'Etudes et
de Recherches Sociales et le
Développement LASDEL,
Niger



Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa
Magonjwa ya Binadamu
(NIMR), Tanzania



Ministry of Public Health
MoPH, Niger



Wizara ya Afya na Ustawi
wa Jamii (MoHSW), Tanzania



United Nations
Population Fund UNFPA,
Niger



Uboreshaji wa Afya ya Uzazi
Tanzania na Niger



Picha kutoka IntHEC, Tanzania



Namna ya mawasiliano

Tovuti: www.inthec.org Barua pepe: inthec@liv.ac.uk

Consortium Coordinator, LSTM, Pembroke Place, Liverpool, L3 5QA, England

Tel: 00 44 151 705 3139

Ushirikiano wa Sekta za Afya, Elimu na Jamii:

Mkakati unaongozwa na taarifa za kitafiti katika kuboresha usawa,
ushirikishwaji na ubora wa utoaji wa huduma za afya ya uzazi

IntHEC ni nini?

IntHEC ni mradi wa miaka 4 wa mpango wa utafiti unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya chini ya mkakati wa program ya 7 unaotekelezwa nchini Tanzania na Niger. Nchi hizi zilichaguliwa kwa ajili ya kuandaa mikakati itakayotoa matokeo yatakayotumika kuboresha utoaji wa huduma za afya ya uzazi kwa vijana walioko ukanda wa kusini mwa jangwa la Sahara.

IntHEC inakusudia kufanya nini?

Huduma duni za afya ya uzazi miongoni mwa vijana ni tatizo linaloendelea kusababisha magonjwa na kuongeza hali ya umasikini kwa watu maskini walioko kusini mwa jangwa la Sahara. Ubora wa huduma za afya ya uzazi kwa vijana zinazotolewa na sekta za afya na elimu umedumaishwa na matatizo mbalimbali yaliyomo ndani ya sekta hizi na kwenye jamii kwa ujumla.

Lengo la IntHEC ni kushughulikia mapungufu hayo kwanza kwa kufanya utafiti na kubuni mikakati thabiti ndani ya sekta ya afya, elimu na jamii.



Lengo

Kuboresha utoaji wa huduma ya afya ya uzazi nchini Tanzania na Niger kwa kutumia taarifa mpya za kitafiti.




Mihimili ya IntHEC

- Utafiti
- Sera
- Ushirikiano
- Mipango
- Uhamasishaji

Dhumuni

- 1) Kubainisha mahitaji ya afya ya uzazi ya vijana wa umri wa balehe ambayo hayajafikiwa
- 2) Kutengeneza hafua kushughulikia mapungufu na matatizo yaliyobainishwa
- 3) Kutathmini utekelezaji na matokeo ya hafua kwenye afya ya uzazi kwa vijana
- 4) Ubora, upokeaji na usawa
- 5) Kuimarisha ushirikiano, utafiti na sera katika kuandaa huduma zinazowezekana za afya ya uzazi bila ubaguzi wa kijinsia

Mpango kazi (2010-2014)



Matokeo yanayotegemewa

- Sera mpya kuhusu ufahamu wa Afya ya uzazi kwa vijana
- Taarifa za kitafiti kuhusu mikakati ya afya ya uzazi katika sekta ya Afya Elimu na Jamii
- Ushirikiano mpya ulio imara kwa ajili ya uboreshaji, utoaji na upatikanaji wa huduma ya afya ya uzazi kwa vijana

